- tuta V** (1) kauka (*dry up*): **Chungu cha tona kitutu.** Chungu cha kiasi kikuu kimekauka. **Vanangojwa vatute njo vajengwe.** Panasubiriwa kukauka ndipo pajengwe. (2) toka jasho (*sweat*): **Umande uoko ye kanatuta jasho.** Baridi iliyoko yeye anatoka jasho.
- tutua V** kumwumiza kigori kwa kumwingilia mbele (*rape a small girl*): **Naima katutulwa nyi Hija.** Naima ameingiliwa na kuharibiwa na Hija. **Naima halitutuka ja avyotutuka Nasra.** Naima hakuharibika kama alivyoharibika Nasra.
- tuwale** chuwale (*scallop living in sea*): **Tuwale zizojabaki zuzwa.** Chuwale zilizobakia zimeuzwa.

- twal(a) V** chukua, pkea (*fetch, carry, receive*): **Nyimba akatwaa.** Nimempa akapokea. **Cha panga sitwale.** Cha mbali usichukue.
- twanga V** (1) twanga (*pound*): (2) piga (*hit, beat*): **Chakutwanga miti.** Nitakupiga bakora.
- tyetyetye** isiyohesabika (*which cannot be counted*): **Nga njavyovata tyetyetye ya mapesa, sinywi ulevi.** Hata kama nitapata mapesa yasiyo idadi sitakunywa.
- ubambakunja** mwanya, kitulizo, wasaa (*gap, hole; room, space, leisure, opportunity*): **Nvyovata ubambakunja tu njo nvyokwenda konana naye.** Kwa kupata wasaa mchache tu ndipo kwenda kuonana naye. **Mgonjwa kavata ubambakunja kachagamii kiwambaza.** Mgonjwa kapata mwanya akaegemea kwenye ukuta.
- ubavu** upande (*side*): **Hamba akae ubavu uowo.** Alitaka kukaa upande huo huo.
- ubeto** mbavu (*side, flank*): **Kiya nyama mnachinjwa, ye huchaka ubeto.** Kila achinjwapo mnyama, yeye hutaka mbavu.
- ubite** uwanagenzi (*state of being under instruction*): **Kanatetema kwa ubite.** Anatemeka kwa uanagenzi.
- uchamizi** uhamiaji, mhamo (*migration*): **Uchamizi uoja ukachakwa haulitendeka.** Ule mhamo uliokuwa ukitakiwa haukuwa.
- uchao** kesho kutwa (*the day after to-morrow*): **Hausi ya Mwanaisha hamba iwe uchao.** Arusi ya Mwanaisha itakuwa kesho kutwa. **Uchao chawa mgeni wako ko.** Kesho kutwa nitakuwa mgeni wako huko.
- uche** (1) kumekucha (*sun has risen*): **Tuvyokona uche njo tuvyolawa nje.** Kwa kuona kumekucha ndipo tulipotoka nje. (2) njaa ya mtoto ambaye mama yake mjamzito (*hunger of a baby whose mother is pregnant*):
- uchezi** (1) harufu ya maziwa (*smell of milk*): **Nguo izo zinanuka uchezi.** Nguo hizo zinanuka harufu ya maziwa. (2) harufu ya maganda ya ndimu, chungwa n.k. (*smell of the skin of citrus fruits*):
- uchokoo mi-** mchokoo (*pointed stick for digging cuttlefish*): **Ama kevu na uchokoo, ngavata nyambo wengi.** Alau alikuwa na mchokoo, angaliwapata pweza wengi.
- uchozi** uchongaji (*carving*): **Uchozi njo kazi yakwe.** Uchongaji ndiyo kazi yake. **Wana wanafundwa uchozi.** Watoto wanafundishwa uchongaji.
- uchwejua** magharibi (*the west, direction of sunset*): **Hasumkia uchwejua soneke.** Nikikimbilia upande wa magharibi sitaonekana.
- udi V** rudi (*come back, return*): **Tukaudi tuchawa kukoko.** Tukirudi tutakuwa kuko huko. **Uchavyoudi njo nchavyokuka.** Utakaporudi ndipo nitakapokupa.

- udole (ndole)** kidole (*finger*): **Mvulyana mzima, kanatia hina ndoleni!** Mwnaume mzima, anatia hina vidoleni!
- udungusi** ubabaifu, utu (*uncertainty*): **Yasiyomkaza hujitia udungusi.** Kwa yasiyomridhisha hujitia ubabaifu.
- ufyagio mi-** ufagio (*broom*): **Ufyagio uojawa valya uwa?** Ufyagio uliokuwa pale uko wapi?
- ufyagizi** ufagiaji (*sweeping*): **Kufyagia njia so kuokota pesa, kuokota pesa majaliwa.** Kufagia njia sio kuokota pesa, kuokota pesa ni majaliwa.
- ugolo** ulaini (*softness*): **Kiya hauvika kangame, hauna ugolo.** Kila nikiupika mgumu, haulainiki.
- ugondi** mguu (*leg, foot*): **Hamba akodoke ugondi.** Nusura ateteruke mguu.
- ugungu** ukaidi, ukorofi (*disobedience, malignity, brutality*): **Mwana kaudizwa kwao kwa ugungu.** Mtoto karudishwa kwao kwa ukorofi.
- ugunu (ngunu)** ununu (*thatch, roofing grass*): **Asia halichaka kwezekewa ngunu.** Asia hakuridhi kwezekewa nunu. **Mwanaisha hwenda akanunua ngunu za viungo.** Mwanaisha huenda akinunua nunu kwa ajili ya viungo.
- ugwadu mi-** mtu mwembamba sana (*a very thin person*): **Uno ugwadu.** Huyu mwembamba.
- uhambachore** rojo ya chakula, kama vile muhogo, ndizi, magimbi n.k. na kupikwa kwa nazi (*thick gravy*): **Ulya mhogo kauli uhambachore tu.** Kwenye ule muhogo kaila rojo tu.
- uheke** umbea (*tale-bearing, spreading scandal*): **Jambo lya uheke si sana yangu.** Umbea si desturi yangu.
- ujavuko** (1) nafasi ya kupita kwa taabu (*space to pass with difficulty*): **Silivata nga ujavuko wa kungia.** Sikupata nafasi ya kuingia.
(2) njia iliyoachwa zamani na kuanza kuota majani (*old path or road which has started to grow grass*): **Wezeza ujavuko uowo.** Fuata njia hiyo hiyo.
- ujezi mi-** ujenzi (*building*): **Ujezi haulijawako kwa vua.** Ujengaji haukuwako kwa mvua. **Ujezi nao tunafundwa.** Ujenzi nao tunafundishwa.
- ujoma** njaa (*hunger*): **Akana ujoma hamba hashibi.** Akiwa na njaa kama kwamba hashibi. **Ngwambe ane ujoma, heya icho cho hali.** Awe na njaa namna gani, lakini hicho hatakula.
- ujovu** mkundu (*the anus*): **Kana kilezi ujovuni.** Ana harara mkunduni.

uka V	ondoka, nyanyuka (<i>leave, go off</i>): Uka ko. Ondoka huko. Mkauka nami chauka. Mkiondoka nami nitaondoka. Ukani meze. Nyanyukeni basi. Tuuke mahaa vano. Tuondoke mahali hapa. Sasa tuuke va. Sasa tunyanyuke hapa.
ukalo	jiti lenye ncha (<i>a pointed stick</i>): Kamchocho kwa ukalo. Kamchoma jiti.
ukenja	sauti kali ya kupaa (<i>high-pitched voice</i>): Kalavya ukenja hageza kanaupeta. Kapaza sauti nikadhania anakufa.
uko	huko (<i>there</i>): Uko okokwenda siko ko. Huko ulikokwenda siko huko.
ukomba	nyama ya dafu (<i>white part of the coconut</i>): Ye hunywa maji tu, ukomba hawe bu. Yeye hunywa maji ya dafu tu, nyama ya dafu haitaki.
ukoti	kikonyo, kishiko cha tunda (<i>stalk of a fruit</i>): Shelisheli ligwishwa na ukoti wakwe. Shelisheli limeangushwa na kishiko chake.
ukuche	ukucha (<i>nail</i>): Kemena akota kuche. Aanza kuota kucha. Nga ukuche ulawa. Hata ukucha umetoka.
ukungu	alfajiri (<i>time before dawn</i>): Asha na Hassan waja ndawia va na ukungu. Asha na Hassan wamekuja kunijulia hali hapa alfajiri.
ulagaito	gari la senema (<i>a car for showing films</i>): Ulagaitoni kwevu na kachunga. Kwenye senema kumeonyeshwa michezo ya kuigiza.
ulanga	uwanga (<i>plant growing edible roots like sweet potato</i>): Mnjaa ulanga ukawa. Kwa mwenye njaa hata uwanga humkawilia.
ulanifu	ulafi, uroho (<i>gluttony, avarice greediness</i>): Hamba asamwe nyi chinyango kwa ulanifu wakwe. Nusura kinofu cha nyama kimkwame kwa uroho wake.
ulongo	ubongo (<i>brain</i>): Miye nyioja hachaka ulongo. Mimi niliokuwa nikitaka ni ubongo.
umande	baridi (<i>cold</i>): Umande uojawako hamba hawa kichune. Baridi iliyokuweko si wa kukaa mwili wazi. Hamba wafwe kwa umande. Walikurubia kufa kwa baridi.
umanja mi-	boriti ya mlango (<i>beam of the door</i>): Ulya umanja uzwa. Ule ubao (wa mlango) umeuzwa. Umanja njo uwozikiwa maiti. Ubao wa mlango ndio uliozikiwa maiti.
umbi	vumbi; udongo (<i>dust, clay</i>): Umbi wa Kae u wakundu. Udongo wa Makunduchi ni mwekundu. Nguo ziwatii kwa umbi. Nguo zimechafuka kwa vumbi.
umia	mafua (<i>bronchitis</i>): Akamiza umia hulawa machininga. Akipenga mafua hutokwa na damu puani.

unazi	uharibifu (taz. nanga):
unazi	ubadhirifu (<i>extravagance, prodigality</i>): Unazi uotendwa avo haujalawia. Ubadhirifu uliofanywa hapo haujapata kutokea.
unda V	fanya, tengeneza (<i>do, make</i>): Waoiunda wamejifwia kale tu. Walioifanya wamekwisha kufariki zamani sana.
unduka V	inuka, tutumka (<i>raise, get up</i>): Valya mahaa vaunduku. Mahali pale pameinuka.
ungua V	peta na kusanya kwa kuzungusha ungo (<i>sift and collect by winnowing the winnowing tray</i>):
unju	asubuhi (<i>morning</i>): Afua kazitoo gari za unju. Afua amezikosea gari za asubuhi. Jua lipatwa va na unju. Hapa jua limepatwa asubuhi.
unywili	unywele (<i>hair</i>): Dau kaokoto unywili wa shetani. Dau ameokota unywele wa shetani. Unywili njo karogewa. Akarogewa kwa unywele.
upambazi	pambazi, mbavu (<i>flank</i>): Sichana kanavukutwa nyi upambazi. Sichana anaumwa na mbavu.
upamboni	wekwa ndani muwele (<i>being confined inside</i>): Naima kawa upamboni. Naima alikuwa katika hali ya kupambwa (kwa ajili ya kupigiwa ngoma kwa sababu ya kusawariwa na shetani).
upenu	baraza (<i>verandah</i>): Juma kapweteka upenuni. Juma kakaa barazani.
upope	upumbavu (<i>stupidness</i>): Nga upope wakwe unatenda shaki. Ama upumbavu wake unakera. Vano hachowezwa, mana kapopo. Hapa hatasemeshwa, maana kapumbaa.
upwatara	uharo (<i>loose stools</i>): Upwatara kaukobaga Maasa. Maasa kajitapakaza uharo. Hunge lyevu likalya upwatara yavo. Mbwa alikuwa akila uharo hapo.
usaganani	unga wa sembe (<i>maize flower</i>): Isa usaganani umchwagisi. Isa limemharisha sembe.
usalida	utamu (<i>sweetness</i>): Mwezenu, ulya mtoli siliutambua, mwadu njonee usalida tu. Hakika lile tunda sikulijua isipokuwa nimejionea utamu tu.
usavu	mapuuza, uzembe (<i>slackness, idleness, indifference</i>): Vilya vyakulya vinangiki kwa usavu. Kile chakula kimeharibika kwa uzembe. Kaitoo kwa usavu wakwe. Ameikosa kwa mapuuza yake.
usesea	sehemu ndogo, kipande (<i>small part, a bit</i>): Usesea aokukwa kaufuku. Sehemu aliyopewa hakuithamini.

- ushengazi** makumbi machanga ya dafu, mashushu ya dafu (*fibre of the coconut fruit*): **Kwa ujoma nga ushengazi hugwenya.** Hata makumbi machanga hung'ong'ona kwa njaa.
- usheza** mchezo (*play*): **Mzale kapigwa kwao kwa usheza.** Mzale amepigwa kwao kwa mchezo. **Akawa ushezani nga humgeze.** Wala humdhanii akiwa mchezoni. **Sishikenamia usheza tu.** Usishiriki michezo tu. **Ulya njo usheza uomkaze Mvyale.** Huo ndio mchezo aupendao Mvyale.
- ushwa (mashwa)** kuti lisilosukwa (*unplaited palm leaf*): **Kaagaa mashwa.** Akachukua makuti yasiyosukwa.
- ushwalala** mstari wa kuchorwa (*a line drawn*): **Vanavo ushwalala njo mtemo.** Penye mchoro huu ndipo mfunda.
- ushwashu** iliyochakaa, epesi (*worn out*): **Lete ushwashu wa kanzu.** Lete kanzu iliyochakaa. **Nyivwae jaje ushwashu uno?** Nivae vipi kanzu hii iliyochakaa?
- usiifu** ukhabiti, uovu, ubaya, ufisadi (*badness, vice, viciousness*): **Usiifu aoutenda, tugeze hachavachaka tena.** Uovu alioufanya tulidhani hatapataka tena. **Mwanaisha hamba achwe kwa usiifu wake.** Mwanaisha alikaribia kuachwa kwa ufisadi wake.
- usindizi** usingizi (*dream*): **Hamvata usindizi va kwa titivuu.** Hapa hamtalala kwa kanyakanya. **Mazi njo kwaza avate usindizi.** Mazi ndio wa kwanza apate usingizi.
- usivi** ufizi (*gum*): **Nyafu kajitogo usivini.** Nyafu amejichoma kwenye ufizi. **Rukia kanalawa damu usivini.** Rukia anatoka damu ufizini.
- usoni** mbeleni (*in front*): **Kumchoweza yakwe yo heti umkalie usoni.** Kusemeshwa yake huyo mpaka mbeleni.
- usoto** kinyume, ovyo (*in opposite way, carelessly*): **Uyo usoto njo sana yakwe.** Ni desturi yake kujibu ovyo.
- usowe** kiwi, haya, tahayuri, kimasomaso (*shame, act of trying to get out of a tight corner by trickery*): **Wajajilavya usowe wo tu.** Hao wamekuja kujitoa kimasomaso.
- usubu** usubi (*a small biting gnat, midge, sandfly*): **Nguuwe kanang'ong'wa nyi usubi.** Nguruwe anazingwa na usubi.
- usufuri** uzi wa chuma (*iron thread*): **Nyoropa kafu kwa usufuri.** Chui amekufa kwa uzi wa chuma.
- usugunufu** usugu (*hardness*): **Ukashikenamia kumpiga tu kuchamtia usugunufu yo.** Ukishiriki kumpiga huyo, utamfanya awe sugu.

uta	1. uzi wa keekee (<i>string of a bow-like bore</i>); 2. haramu (<i>unlawful</i>): Mali ya uta hwenda kwa uta. Mali ya haramu huenda kwa haramu.
utaji	shabaha (<i>aim, target</i>): Wende jifunda utaji. Wamekwenda kujifundisha shabaha. Fatuma njo mwawa utaji. Fatuma ndiye mwenye shabaha.
uteku mi-	mkono, mshikio (<i>hand, handle</i>):
utigiri	uti wa mgongo (<i>backbone</i>): Fatuma kanawangwa nyi utigiri. Fatuma anaumwa na uti wa mgongo.
uto	uamshaji wa daku (<i>waking for 'daku' early in the morning, during Ramadhan</i>): Watenda uto namba jana hawalivita. Nadhani waamshaji wa daku jana hawakupita.
utufwani	upepo (<i>wind</i>): Utufwani uojawako, nga hatuligeza ama tuchafika. Hatukutaraji kufika kwa upepo uliokuweco.
utui mi-	urojo (<i>slackness</i>): Muhidini, utui umpalii. Rojo inampalia Muhidini.
uvisi	upishi (<i>cooking</i>): Wavisi waoja wako hamba vyakulya haviwa ja vilya. Kwa wapishi waliokuwako haiwi chakula kuwa namna ile.
uvundo mi-	harufu mbaya (<i>bad smell</i>): Ulya uvundo unyiwangisi kichwa. Ile harufu mbaya imeniumiza kichwa. Kiambo kihamwa kwa uvundo. Mtaa umehamwa kwa harufu mbaya.
uvupu	upupu (<i>the mucuna bean with irritating glossy hairs</i>): Zainab kanawawigwa nyi uvupu. Zainab anawashwa na upupu. Hamba ane utu kwa uvupu. Alikaribia kuwa chakaramu kwa upupu.
uvwi	uvi, nyigu, mavu (<i>a biting insect resembling the bee</i>): Daudi kanasumka uvwi. Daudi anakimbia manyigu.
uwego	ubavu, upande (<i>side</i>): Uwegoni va kitanda. Pembeni pa kitanda.
uwele (ndwele)	radhi (<i>illness, disease</i>): Vano va vana ndwele. Hapa pana maradhi.
uza V	(1) uliza (<i>ask</i>): Hassan njo mwatuza. Hassan ndiye aliyetuuliza. Nyiuzu heya silikwamkulwa. Nimeuliza lakini sikujibiwa kitu. (2) uza (<i>sell</i>): Nyulizwa ilya kwa shilingi kenda. Nimeuziwa kwa shilingi tisa.
uziwi	utundu, uharabu, uchokozi (<i>mischief, slyness, teasing, annoyance</i>): Tuwani hutenda uziwi akesa akasumka. Tuwani hufanya uchokozi kisha hukimbia. Avyoja akatogoa yo kwa uziwi. Alikuwa akikomoleka mno kwa uharabu wake.
uzumbuzi	kuzurura (<i>going around, walk aimlessly</i>): Rukia kana haha kwa uzumbuzi. Rukia ana njaa kwa kuzurura.

uzumui	upepo uvumao na kuzunguka kwa kasi (<i>cyclone</i>): Ulya usufi utipanywa nyi uzumui. Ule usufi umetawanywa na upepo unaozunguka.
vakata V	pakata (<i>hold e.g. a child on the knee, lap or shoulder</i>): Suleiman heki kuvakata mwana. Suleiman hajui kupakata mtoto.
vangatia V	kumbatia (<i>embrace, clasp in the arms</i>): Kumvangatia kakutwa nyi oga. Kaogopa kumkumbatia. Asishikenamia kuvangatia yo tu. Asipendelee kunikumbatia tu huyo.
vapa V	(1) tafuta (<i>seek, look for</i>): Nani yulya mwaja akavapwa? Ni nani yule aliyekuwa akitafutwa? Msizivapa kachauka vivyo. Asiyezitafuta ataondokea patupu. (2) vuja maji (<i>leak water</i>): Madamu mtungi uo unavapa usitulwe kati. Madhali mtungi huo unavuja maji, usiwekwe ndani.
vata V	pata (<i>get</i>): Kumevata, tuiise tena. Umeshapata, tupishe basi. Kisichovatika leo ngoja uchao. Kisichopatikana leo subiri kesho kutwa.
vavanya V	paraganya, korofisha (<i>spoil, bring to ruin, treat with cruelty</i>): Mkanvavanya mchauka vivyo. Mkiniparaganya mtaondokea patupu.
veleka V	peleka (<i>send</i>): Kaveleka madomboni. Kapeleka makaburini.
venya V	penya (<i>go through</i>): Walya waovenya pya wagwiwa. Wale waliopenya wote wamekamatwa. Tono kwa kuvenyeweza tu. Tuliona kwa kupenyeweza tu.
vepe ma-	mapepe, epesi (<i>light</i>): Tangu achwe vepe. Tangu alipoachwa mwepesi/kakonda.
veu	ukumbi (<i>sitting room, lounge</i>): Kaani vano veu. Kaeni hapa ukumbini.
vevi	mahali karibu (<i>a nearby place</i>): Wende ivo vevi, wanaudi sasa va. Wamekwenda hapo karibu, watarudi sasa hivi.
veza V	nyima (<i>deprive, refuse, not give, esp. of what is due</i>): Wakanveza nawangasa. Wakininyima nitawafukuza. Ngwambe avezwe, heya alye nao. Yuradhi anyimwe lakini ale nao.
vi	pi? (<i>which?</i>): Kachaguu vivi? Amechagua vipi? Yuvi mwakukaza? Ni yupi aliyekupendeza? Waketwe wevi? Wakaitwe wepi? Ivi ayojavakata? Aliipakata ipi? Ame konjo yevi? Ame kaonja yepi?
vidwidwi	(1) alama za maji yapatayo moto (<i>signs of boiling in water</i>): (2) kama maji kwa mbali kwa ajili ya jua kali (<i>looming, reflection of light, illusion</i>):
vifuta	nongwa (<i>disagreeableness, a secret grudge</i>): Akana vifuta hatugomana. Akiwa na nongwa hatuwezani. Mna vifuta asende ko. Mwenye nongwa huko asiende.

vika V	pika (<i>cook</i>): Asha njo kwaza ajifunde kuvika. Asha ndio anaanza kujifunza kupika. Avyovika Asani nga havilivikika. Alivyopika Asani kabisa havikupikika.
viko?	wapi? (<i>where?</i>): Hassan kende viko? Hassan amekwenda wapi? Wevu viko? Walikuwa wapi?
viligisa V	ghasi (<i>confuse, complicate, bustle</i>): Sina nlyotambua kwa kuviligiswa. Sikujua lo lote kwa kughasiwa.
vimbuguyu	shida, mashaka, dhiki (<i>difficulty, doubt, problem</i>): Kemekuta vimbugugu tangu mweke jana. Amepata shida tangu mwaka jana.
vinya V	bimba (<i>lull</i>): Avyovijua kumvinya mwana. Anavyojua kumbimbua mtoto. Nga ajavyovinywa yo halala. Hata kwa kubimbiwa huyo hatalala.
Vinyakanyaka	vitu vya aina mbalimbali (<i>various kinds of things</i>): Kiya wakaja huja na vinyakanyaka. Kila wakija hapa huja na vitu mbalimbali.
visa V	pisha (<i>cause to pass, let pass, allow passage</i>): Amri na Ame hawanakawa kuvisa. Amri na Ame hawakawii kupisha.
vita V	pita (<i>pass by</i>): Vilya kunachungia ye kanavita. Pale unachungulia yeye ndio anapita.
vitisa V	pitisha (<i>let pass, cause to pass</i>) (taz. visa): Kiya vakana watu ye hujivitisa tu. Kila pakiwa na watu yeye hujipitisha tu.
viviga V	ficha, bania; vurugusha; haribu (maneno) (<i>press, hide, mix</i>): Afua, kiya akachowea maneno huyaviviga. Afua, kila asemapo maneno huyabania.
vojea V	kwenda chini (taz. bojea); bonyea (<i>go in a low position, be dented with pressure</i>): Kulya mahaa twebu tukavojea. Tulikuwa tukienda na kubonyea.
vokea V	pokea (<i>receive</i>): Ngwambe akoswe heya simvokee. Hata kama akinuna lakini sitampokea.
vonda V	angukia, elemea (<i>fall upon, go anywhere with a rush</i>): Ukani ko msije vondwa. Huko ondokeni msije mkaangukiwa. Yulya nanuhuyu kafu kwa kuvondwa nyi kiwamba. Yule mtu amefariki kwa kuelemea na kiambaza.
vonoa V	piga, tia adabu (<i>beat, teach good conduct by punishing</i>): Ukamtonisa yo kanaja kuvonoa. Utakapomtonisha huyo atakutia adabu.
vopya	pote (<i>everywhere</i>): Vakumbe vopya vo. Pafagie pote hapo.
vu	kwa ghafla, papo (<i>suddenly, instantly</i>): Vu kwa vu ta. Isiwe papo kwa papo. Ama si kulawiwa vu, wasingegonwa. Lau si kwa kutokewa kwa ghafla, wasingefumaniwa.

- vua** mvua (*rain*): **Ikakuta vua yo ichanangika.** Itakaopata mvua itaharibika. **Mkayacha vuani ichatota.** Mtakapoiacha mvuani itaroa.
- vukuta V** uma (*bite*): **Vakachekenulwa humvukuta.** Pakiwambuliwa humwuma.
- vukutwa V** umia, umwa (*feel pain, be ill, suffer, ache*): **Mvonoe hasa avukutwe.** Hebu mtie adabu aumwe. **Maasa hamba ane utu kwa kuvukutwa.** Nusura Maasa aharibike akili kwa kuumwa.
- vuliza V** puliza (*blow with the mouth, puff*): **Sichana kanavukutwa nyi kemo kwa kuvuliza.** Sichana anaumwa na mashavu kwa kupuliza. **Chokani kuvuliza.** Acheni kupuliza.
- vumbujuka V** Vrudia uzima kwa mahala palipovimba (*regain health, e.g. of swelling or boil*): **Dicho lyakwe limena likavumbujuka sasa.** Jicho lake sasa linarudia hali ya uzima.
- vumilia V** stahimili (*endure, persevere, be patient*): **Wambiwe wo, wasivyovumilia hawapoo.** Wambieni hao, wasipostahimili hawatapona.
- vuna ma-** sega (*honeycomb*): **Ndachuja ta mavunani.** Nakwenda kuchuja nta kwenye masega.
- vunga V** zonga, funga (kwa shuka, mkeka, busati, jamvi n.k.) (*tie inside stg, e.g. sheet, mat etc.*): **Dau akafika vimena vikavungwa.** Dau alipofika (vitu) vimo kuzongwa.
- vusa V** vusha (*cause to cross*): **Sheti avuswe na ukungu.** Yapasa avushwe alfajiri.
- vuuga V** vuruga (*stir up, stir round, excite, exasperate*): **Kapondwa akavuugika.** Kapondwa akavurugika.
- vuvuga V** athiri sana (*influence much*): **Kamvuvugu ja nyambo.** Kampiga kama pweza (sana).
- vuza V** lainisha (*make thin, smooth, flexible*): **Mhogo ukauvuza tia maji.** Muhogo ukiulainisha tia maji.
- vwaa V** vaa (*dress, be dressed, wear clothes*): **Isa hajesavwaa mchonga.** Isa hajaishavaa njuti. **Mzale kanamvwisa Mazi mbwanga.** Mzale anamvisha Mazi suruali.
- vwaga V** chemka (*boil, intr.*): **Akauka vitumbo unga vimena vwaga.** Alipoondoka viazi vidogo vimo kuchemka.
- vwaju** kazi ya kufua nguo zilizooshewa maiti (*act of washing clothes which have been used for cleaning a corpse*): **Watu wende vwaju.** Watu wamekwenda kuosha nguo zilizooshewa maiti.

- vwavwamka** V sitawi (*prosper, flourish, succeed*): **Mhogo uvwavwamku mani.** Muhogo umesitawi majani.
- vwaza** V chemsha (*boil, tr.*): **Vwazani nga tona njo muuke.** Chemsheni walau viazi vikuu ndipo mwondoke.
- vwende ma-** papai (*pawpaw fruit*): **Komba kevu akalya vwende bigilini.** Komba alikuwa akila papai kwenye bigiri. **Lilya vwende mwalishoba Mazi.** Aliyelila lile papai ni Mazi.
- vyaa** V zaa (*give birth, bring fruit*): **Mwanaisha njo kwaza avyaaye mwana mwanamke.** Mwanaisha ndio kwanza azae binti. **Tumeovyaa pya wamelolwa.** Tuliowazaa wote wameshaolewa.
- vyalo ma-** kizazi, zao, uzazi (*birth, pregnancy*): **Vyalo limshiki.** Uzazi umeshika (haishi kuzaa). **Vyalo limondese.** Uzazi umemkondesha.
- vyeza** V kuwa mzima (*be healthy*): **Leo silivyeza.** Leo mimi si mzima.
- vyoga** V pita pasipo njia (*go in a place where there is no way or path*): **Walya watu wangii uvupu kwa kuvyoga tu.** Wale watu wameingiwa na upupu kwa kupita msimokuwa na njia.
- vyogovyogo** homa isiyo na mahali maalum (*fever all over the body*): **Tangu nyivyolamka na vyogovyogo.** Tangu nilipoamka nina homa.
- vyongoa** V sokotasokota, nyonganyonga, piga mapindi (*keep twisting, spinning*): **Ukamwona kanajivyongoa we usende.** Ukimwona ajipiga mapindi, wewe usiende.
- vyungu** alama za jasho kukauka mwilini (*marks of sweat drying on the body*): **Hamdu hogo heti ane vyunyu maungoni.** Hamdu hakogi mpaka awe na alama za jasho mwilini.
- vyuno** viuno (*loins, flanks*): **Wachanjwa vyunoni.** Wamechanjwa viunoni.
- vyuvyuza** V tia uvivu (*influence others so that they become lazy*): **Suleimani kangaswa kwa kuvyuvyuza weziwe.** Suleimani amefukuzwa kwa kuwatia uvivu wenziwe.
- wadi** bin (taz. **adi**) (*son of*).
- wagaa** V chukua kwa kukumbatia (*take by lifting onto arms*): **Mabwe hayanawagalika.** Mawe hayachukuliki kwa kukumbatia.
- wage** majani yanayowasha, weni, mavi ya nyanya (*irritating grass, weed*): **Ulya wage ung'olwa pya kondeni.** Ule weni umeng'olewa wote kondeni. **Hamba walie kwa wage.** Nusura walie kwa mavi ya nyanya.
- wana** V pambana (*compete*): **Kawana akamgoma.** Kapambana naye akamshinda.

- wanda V** katakata, charanga (*cut in pieces*); kulima msitu kwa kuutengeneza ili uje uwake vyema (*prepare a forest so that it catches fire easily for clearing the area for cultivation*): **Kama huliwanda msitu hawaka to.** Kama hukuucharanga msitu hauwaki vizuri. **Yayo matambi yawande tupange tanu ya makaa.** Hayo matawi yakatekate tupange tanu ya makaa.
- wanga V** (1) kuwa na maumivu, umwa (*have pains, suffer*): **Akawangwa nyi kichwa akadalie.** Aumwapo na kichwa mwache akalale. (2) vunja (*break*): **Mchaiwanga ailipe.** Atakayeivunja ailipe.
- wapa V** tafuta (*seek, look for*): **Iwapwa hata hailikoneka.** Ilitafutwa sana haikuonekana. **Zilya njanakee ziwapwa hata.** Vile vitoto vilitafutwa sana.
- wapwa** pwanipwani (*shore, coast*): **Tuviti wapwa kusumka jua.** Tulipita pwanipwani ili kukimbia jua.
- wavuka V** pita pasipokuwa safi, pwasha (*pass in untidy places*): **Twevu tukawavuka tu kwa ugeni.** Tulikuwa tukipita pasipokuwa safi kwa ugeni.
- wawa V** washa (*burn; irritate*): **Mnawawigwa kwa kuwavuka tu.** Mnawashwa kwa kupwasha tu. **Majani ayo yanawawa.** Majani hayo yanawasha.
- wawawawa** vurumai, vurugu (*disorder*): **Pindi zilya njonee wawawawa tu valya.** Wakati ule nilijionea vurugu tu pale.
- wee** wewe (*you*): **Wee huviji kusoma.** Wewe hujui kusoma. **Wee kumekulya?** Wewe umekula?
- wegoni** pembezoni (*corner*): **Wakawavuka kwa umo wegoni hawachawawigwa.** Wakipwasha kwa humo pembezoni mwa konde hawatawashwa. **Zamani wegoni mwa konde iyoyo.** Jificheni pembezoni mwa konde hiyo hiyo.
- wehu** ukware, ushongo (*carnal lust, uncontrolled lust*): **Hanakaa na mume kwa wehu.** Haishi na mume kwa ukware.
- weka** pekee (*alone*): **Kulala weka kanaoga.** Kulala peke yake anaogopa. **Rukia kakazwa n'kulya weka.** Rukia anapenda kula peke yake.
- wenga V** dhuru (*cause harm*): **Midamu inamwenga na asikwe.** Madhali inamduru, basi asipewe. **Sinawengwa n'kitu.** Hakuna cha kuniduru.
- wesha V** washa moto (*kindle fire*): **Mwaiwasha njo mchaizima.** Aliyewasha ndiye wa kuizima.
- widi V** vunda (*be high, of meat which has been laid by for some time*):
- wina** mtego wa shimo (*pitfall*): **Nguuwe kanasa winani.** Nguruwe amenasa kwenye mtego wa shimo.

- wisha V** ondosha (*take away, remove*): **Isivyowishwa ichataka jua.** Isipoondoshwa itaumia kwa jua. **Mwatua njo mchawisha.** Aliyeweka ndiye wa kuiondosha.
- wivi** (1) kificho cha nyuma ya mlango (*space beyond the opened door*): **Mpaye uojawa wivini wuzwa.** Mtarimbo uliokuwa nyuma ya mlango umeuzwa. (2) wizi (*theft*):
(3) ubao wa juu wa mlango, shubaka la mlango (*a window-like recess above a door*):
- yagaisa V** tafuna (*chew*): **Ugali haunayagaiswa.** Ugali hautafunwi.
- yaya V** unguwa (*get burned*): **Mhindi wachwa hata uyaya.** Muhindi umeachwa mpaka ukaungua.
- yayatika V** lia sana, lalaika (*cry a lot*): **Mwana kemena kwio kwa kuyayatika.** Mtoto kafanya kwikwi kwa kulia sana. **Kuwangwa uko ko, uyo kuyatatika.** Huyo kuumwa huko ni kwa kulia mno.
- ye** yeye (*he/she/it*): **Akamona nyoka ye husumka.** Akimwona nyoka yeye hukimbia. **Nyivyomwambia asende ye halidumba kende tu.** Nilipomwambia asiende yeye hakukubali, alikwenda tu.
- yenga V** (1) tembea, kwenda huko na huko (*move, go, go around*): **Samaki wanayenga demani.** Samaki wanatembeatembea katika dema. (2) tunza (*take care of*):
- yengayenga V** chezacheza (*play, be playful*): **Usiyengeyenge mahakamani.** Usichezecheze mahakamani. **Ukapigwa msondo huyengayenga.** Nikipigwa ngoma huhezacheza. **Akasikia vinanda kuchamona kanayengayenga.** Akisikia mazeka utamwona anachezacheza.
- yogoza V** tia utupa (*put the juice of a species of euphorbia, used as a fish poison*): **Vasivyoyogozwa havavatiki kitu.** Pasipotiwa utupa hapatapatikana kitu.
- zakua V** toka mbio (*leave hurriedly*): **Kazakuu halikutwa.** Amekwenda mbio hakupatikana.
- zama V** jificha (*hide oneself*): **Ngwambe azame kuwa kokosi, heya akakutwa kawa shidani.** Hata kama akijificha kokote kule, lakini akipatikana yumo tabuni.
- zebe ma-** jitu pumbavupumbavu (*a stupid giant*):
- zezeta ma-** siokuwa na haja, ovyo (k.v. maneno) (*thing or matter which is not needed*):
- zi** nzi (*fly*): **Zi kwa kidonda mbaa.** Nzi kwa kijeraha yu mbaya. **Vuai kali zi.** Vuai amekula nzi.
- zida V** shinda (*win, be superior*): **Akanzidi sichakaa.** Akinishinda sitakaa.

- zido** hali ya kuzimia (*state of being unconscious*): **Ilya koroma iyojampiga kende ga zido.** Kile kidaka kilichompiga alizimia kwanza.
- zigua V** tumia (*use*): **Nga mwenyuwe hajaizigua.** Hata mwenyewe hajaitumia.
- zima** nzima (*whole, healthy*): **Zija ja vivivi zimazima.** Zimekuja vivi hivi nzimanzima.
- zima V** zima (*extinguish*): **Wakaizima wachakwagaswa.** Wakiizima watafukuzwa.
- zimnga V** subiri (*wait*): **Hazimnga njo nchavyozivata leo.** Nikisubiri ndipo zitakapozipata leo.
- zizia V** vizia (*frustrate, spoil work for, keep an unfriendly eye on, molest, harass*): **Msishikenamia kuzizia tu.** Msishiriki kuvizia. **Ngwambe asivate heya vyo azizie.** Hata asipate kitu lakini hataacha kuvizia.
- zozoa V** zongoa (*unwind*): **Ngwambe nsiinune heya nyiwe nyiizozoo.** Haidhuru nisiinunue lakini niwe nimeizongoa.
- zumbua V** zubaa, zurura ovyo (*be astonished, be caught by a condition of not knowing what to do*): **Nawangwa n'kichwa kwa kuzumbua juani.** Naumwa na kichwa kwa kuzurura juani.

UTANGULIZI

Kabla sijaeleza mengi ninayokusudia kuhusiana na kamusi hii, kwanza napenda ifahamike kwamba lugha ninayoizungumza humu kitabuni inatokana na lugha ya Kiswahili. Na kwamba hicho Kiswahili ni miongoni mwa kugha kuu zinazozungumzwa na wengi mno ulimwenguni siku hizi. Kila uchao ufahasa wa lugha yenyewe unazidi kuenea na kupata kuongewa na wengi. Isitoshe, licha ya hao wengi wanaoiongea lugha hiyo, ni dhahiri kuwa hata si wenyeji wa lugha yenyewe wengi wetu tuna lahaja zetu za kiasili. Pili, katika upwa wa Afrika ya Mashariki lugha ya Kiswahili ndiko kwao.

Uamuzi wa Tanzania kutumia Kiswahili kuwa ni lugha kuu ya taifa unatokana na lahaja mbalimbali zenye uasili wa lugha zenyewe. Kwa upande wa Tanzania visiwani, utakuta kwamba kupanuka kwa Kiswahili kuna migawanyiko kadha ambayo hutafautiana kwa uchache sana. Zanzibar visiwani kuna lahaja nne kuu ambazo husemwa na wenyeji hadi hivi sasa. Nazo ni: lahaja ya Kipemba, lahaja ya Kitumbatu, lahaja ya Kiunguja-mjini na hii lahaja ya Kikae, yaani Kimakunduchi.

Kamusi ya lahaja ya Kikae ni changamoto kwa wazungumzaji wa lahaja nyingine za humu visiwani. Kwani sehemu kubwa ya kusini ya Unguja hutumia Kikae na upande wa kaskazini wanasema Kitumbatu. Kikae na Kitumbatu ni lugha ambazo hazikurubiani kamwe na Kiunguja mjini, yaani lahaja iliyosanifiwa. Kwani lahaja mbili hizo zina maneno mengi zaidi yenye asili ya Kiswahili na machache sana ni yenye asili ya kigeni. Ndio kusema kuwa hazikunasibiana kwa vile ambavyo Kiunguja-mjini kimechanganya maneno mengi ya lugha za kigeni kwa kutokana na historia yake.

Kamusi ya lahaja ya Kikae imetengenezwa kwa madhumuni maalumu. Kwanza ni kuwawekea pamoja na kuwadumishia vizazi vya Wilaya ya Kusini kuijua lugha yao ya asili. Sababu ni kuwa pamoja na maingiliano ya jamii nyinginezo utakuta kuwa ndimi za vizazi vilivyotangulia zinahitilafiana sana na ndimi za vizazi vilivyotangulia zinahitilafiana sana na ndimi za vizazi vya siku hizi, seuze hivyo vijavyo. Kwa hivyo msamiati wa lahaja yenyewe usije ukapotee kabisa.

Kamusi hii itawasaidia watu katika mahitaji yao ya kila siku kwenye matumizi ya lugha kwa jumla na katika shughuli nyinginezo, kama vile utafiti. Hivyo walimu, wanafunzi na wataalamu wengine wawe na tegemeo maridhawa ya lahaja ya Kikae katika mazingira yoyote.

Katika Mkoa wa Kusini, hasa Wilaya ya Kusini Unguja, kuna miji kama Pete, Jozani, Kitogani, Bwejuu, Paje, Jambiani, Mungoni, Muyuni, Kizimkazi, Kibuteni, Mtende na Makunduchi yenyewe ambayo ndiyo makao makuu ya lahaja ya Kikae. Basi wenyeji wote humo wana lafudhi zao ambazo hupitana kwa uchache sana. Hata hivyo wananchi waliomo wana mashirikiano ya hali u mali na ambayo ni makubwa katika shughuli zao za kimawasiliano.

Japokuwa kila kijiji kina mahadhi ya aina yake, lakini Kikae ndicho kinachochukua nafasi pana zaidi na kwamba wananchi wote huweza kuwasiliana vyema. Kwa kawaida Wamakunduchi wanapokutana na kuongea faragha hutumia lafudhi yao, yaani Kikae, wakati wanapoongea na wengineo hutumia lugha sanifu.

Haji Chum

Makunduchi, Zanzibar

SHUKRANI

Ni vigumu kwangu kuweza kuwataja kwa majina yao wote wale walionisaidia katika ukusanyaji wa maneno ya kamusi hii, kwani wengi wao hawakujua kuwa ndio wakishiriki wakati huo. Ama wako baadhi ambao wamenisaidia zaidi, kwa hivyo nitawataja majina yao hapa pamoja na kuwashukuru hadharani kwa juhudi zao kubwa zilizodumu mpaka hatua ya mwisho ya utungaji huu.

Pia sina budi kueleza hapa kwamba kadiri ya hitilafu zitakazojitokeza humu ni zangu mimi peke yangu, yaani iwapo ni mafanikio yawe ni ya wote walioshiriki na iwapo ni makosa basi yawe kwangu mimi peke yangu.

Miongoni mwa hao walionisaidia pakubwa ni: Ndugu zangu, Bw. Hassan Chum, aliyekuwa fundi wa kushona Jambiani, Bw. Talib Chum, fundi seremala wa Jambiani, Bw. Bakari Chum, fundi seremala Serikalini na dada yangu Mtumwa Chum wa Makunduchi. Mchango mwengine wa mara kwa mara lilikuwa nikiupata kutokana na wake zangu Bi Subira Haji wa Nganani na Bi Mauwa Askari wa Matazi, wote humu Makunduchi.

Wengine ni Mwalim Seif Makame Ameir wa Mkungwini, Mwalim Ramadhan Makame Ali (Kashibo) wa Mzuri humu Makunduchi pamoja na Dr. T.S.Y. Sengo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hawa ndio walioupitia mswada tangu mwanzo wakinipa mashauri na maelekezo ya kufaa hadi mwisho wake.

Mchango mwengine nimeupata kwa Bw. Sigombe Maalim wa Matazi. Yeye alikuwa akiniita na kunikaribisha kwake ili kunipa meneno mengi ya kiasili kwa ajili ya mswada wenyewe.

Ndipo tena Profesa Arvi Hurskainen wa Chuo Kikuu cha Helsinki, Finland, yeye ndiye aliyechukulia dhamana tangu mswada na kuendeleza mpaka kuwa kitabu kamili.

Kadhalika shukrani zangu nyingi ziwaendee wote niliopata kukutana na kuongea nao katika shughuli zetu mbali mbali za kijamii – tangu za furaha, misiba na pia sherehe nyenginezo. Hapa natoa wito kwamba namkaribisha mtu yeyote atakayezikuta hitilafu zozote anijulishe, ili dosari hizo ziondolewe mara moja.

Mwisho pamoja na misaada mingi niliyoipata sitodai kuwa nimeweza kukusanya maneno yote ya lahaja yenyewe, kwa hivyo mtu yeyote mwenye neno na ambalo halimo humu aniarifu ili liingizwe mara tu kitabu kitakapokwenda kuchapwa mara nyengine. Kwani kufanya hivyo ndivyo tutakapoweza kuihifadhi lahaja yetu kwa ajili ya vizazi vinginevyo.

Haji Chum

Makunduchi, Zanzibar

DIBAJI

Napenda kumpongeza Ndugu Haji Chum kwa kazi ngumu sana aliyoifanya katika kutafiti na kukusanya maneno ambayo hasa ndiyo msingi wa Kikae. Lazima nikubali mimi binafsi nisingeweza kuifanya kazi hiyo. Katika kukipitia kitabu hiki cha Kikae, nimekuta maneno ambayo sijayatumia miaka mingi sana, hata naweza nikasema kuwa nimeyasau. Pia nimekumbana na maneno ambayo siyajui. Nilimpa kazi ngumu Ndugu Haji Chum, kazi ngumu ya kunitosheleza na mpaka nikatosheka kuwa hayo maneno yanakubalika. Kwa hivyo mimi mwenyewe nimejifunza mengi kutoka katika kitabu hiki.

Kikae ni Kiswahili ambacho husemwa huko Makunduchi, yaani Kae. Lakini ndani yake yamo maneno mengi sana ambayo hayana asili ya Kiswahili. Inawezekana maneno hayo yameazimwa kutoka katika lugha kadha zisemwazo Tanzania Bara, Kenya na kwingineko. Vile vile ni shida sana kwa mtu ambaye hakuzaliwa na hasa kukulia Makunduchi kuweza kukisema kwa fasaha nzuri. Watu wengi hujaribu kukisema lakini mara hushindwa katika matamshi. Kwa sababu hiyo baadhi ya watu hufikiri kuwa Kikae ni lugha tofauti na Kiswahili.

Pengine mwandishi hatoishia hapo tu. Labda katika kitabu chake cha pili atafanya utafiti zaidi juu ya asili ya baadhi ya maneno na pia atafanya utafiti juu ya kukisema na kukitamka vizuri hicho Kikae.

Hii ni kazi ngumu na nzito; lakini hapana shaka kuwa mwandishi ameanza kazi muhimu ambayo vizazi vijavyo vinaweza kuiendeleza kwa ufanisi mzuri zaidi.

Idsris Abdul Wakil

Rais wa Nne wa Zanzibar

Zanzibar,

Novemba 1993